



FAIR COMPETITION COMMISSION



TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

FCC YAKAMATA MABOMBA YA MAJI BANDIA

Tume ya Ushindani (FCC), ikifanya kazi kwa mamlaka iliyopewa kwa mujibu wa Sheria ya Alama za Bidhaa ya mwaka 1963, kama ilivyorekebisha, pamoja na kanuni zake za mwaka 2008, mnamo siku ya Jumatano, tarehe 24 Julai, 2013, ilifanya zoezi la ukaguzi wa kushitukiza katika maduka na bohari zilizoshukiwa kuhifadhi na kuuza mabomba ya maji plastiki (PVC) bandia, yenye nembo ya biashara ya IPS katika eneo la Kariakoo.

FCC iliendesha operesheni hiyo kwa kushirikiana na jeshi la polisi na wakala wa Hataza na Miliki Bunifu ya IPS wa hapa nchini, ambaye ni kampuni ya NABAKI AFRIKA.

Operesheni hiyo ilifanikisha ukamataji wa jumla ya mabomba bandia ya maji yapatayo 728 yanayokadiriwa kuwa na thamani ya Sh milioni 8.7. Mabomba hayo yalikatwa katika maduka manne kati ya takriban maduka saba yaliyokaguliwa baada ya kushukiwa kujishughulisha na uuzaji wa bidhaa bandia za mabomba ya maji ya plastiki.

Maduka yaliyokamatwa na mabomba bandia ya IPS pamoja na idadi ya mabomba husika ni kama ifuatavyo:

Na.	Duka/Mmiliki wa Duka	Idadi
1.	Nicas August Ngallo, Hardware Building Materials S.L.P. 22110, DSM	97
2.	Sospeter Deus Mashauri S.L.P. 227, DSM	56
3.	Zamzam Ltd. S.L.P. 79896, DSM	504
4.	Shaban Omar Mnenke, S.L.P. 72639, DSM	71
	JUMLA	728

Zoezi hilo la ukaguzi na ukamataji wa bidhaa bandia husika lilitokana na lalamiko la mwakilishi wa kampuni ya IPS, Kampuni ya NABAKI AFRICA alililoliwasilisha katika Tume ya Ushindani kupitia barua yake ya tarehe 26 Juni, 2013 ikiainisha uwepo wa bidhaa bandia zinazouzwa kwa kuigiza nembo ya IPS, kinyume na Kifungu cha 6 cha Sheria ya Alama za Bidhaa ya mwaka 1963, iliyorekebishwa katika baadhi ya maduka ya vifaa vya ujenzi yaliyopo eneo la Kariakoo.

Aidha, kampuni ya IPS yenye makazi yake nchini Argentina, kwa kushirikiana na wakala wake, NABAKI AFRIKA, ilifanya uchunguzi wa kina katika soko la Tanzania na kuchukua sampuni za mabomba bandia kwa ajili ya uchunguzi wa maabara. Taarifa za uchunguzi wa maabara kuhusu mabomba hayo zimebainisha kuwa mabomba hayo bandia pia hayakidhi viwango vya ubora na hivyo si salama kwa matumizi ya kupitishia maji kwa matumizi ya binadamu.

Wamiliki wote wa maduka yaliyokutwa na bidhaa bandia husika wamepewa Notisi ya kukamatiwa bidhaa zao. Bidhaa hizo zimehifadhiwa katika bohari ya Serikali. Aidha, wametakiwa kuchukua hatua stahiki kwa mujibu wa sheria ya alama za bidhaa na kanuni zake kutokana na kadhia hiyo ya kujishughulisha na biashara ya bidhaa bandia.

Zoezi la ukaguzi wa kushitukiza na ukamataji wa bidhaa bandia za IPS ni sehemu ya juhudi za Serikali katika kuhakikisha kuwa Tanzania haigeuzwi kuwa jalala la bidhaa bandia na hafifu. Vita dhidi ya bidhaa bandia vinalenga pia kuwalinda walaji wa Tanzania dhidi ya nia ovu za wafanyabiashara wasio waaminifu ambao huwadaa kwa nia ya kuwaibia fedha zao bila kuwa na madhumuni ya kuwapatia bidhaa zinazofaa kwa matumizi tarajiwa.

Pamoja na utekelezaji wa sheria, Tume ya Ushindani inatoa rai kwa wamiliki wa hataza na miliki bunifu za bidhaa kuongeza bidii ya kuwaelimisha wasambazaji na wauzaji wa bidhaa zao kuhusu namna bora ya kujihadhari na kutambua bidhaa bandia zinazokiuka hataza na miliki bunifu husika ili waweze kuwasaidia walaji kupata bidhaa halisi na zisizohatarisha maisha ya mlaji wa Tanzania.

Msako dhidi ya wafanyabiashara wanaojihusisha na biashara ya bidhaa bandia ni suala endelevu na hivyo tutawasaka na kuwachukulia hatua wale wote wanaojihusisha na biashara ya bidhaa bandia.

Alama ya biashara ya IPS imesajiliwa nchini na mamlaka husika tarehe 4 Septemba, 2009 kwa namba 29936 katika daraja la 17.

Imetolewa na Kitengo cha Mawasiliano na Mahusiano ya Umma

Alhamisi, Julai 25, 2013.

Tume ya Ushindani

Ghro ya Pili, Tawi la Magharibi, Ubungo Plaza, Br. ya Morogoro,
S.L.P 7883, Dar es Salaam.

Kwa maelezo zaidi wasiliana na **Frank S. Mdimi, Afisa Mwandamizi, Mawasiliano na Mahusiano ya Umma** kwa Namba MEZANI:+255222461565, 2461566, 2461568, 2461569; NUKUSHI:+255 222461567; Mkononi: +255784762437 na +25573944083, Barua Pepe: info@competition.or.tz au fmdimi@competition.or.tz.